



mondia.

Mondia Pay yapanua fursa mpya za fintech ili kuongeza uwezo wa kufikia huduma ya burudani dijitali kwa wateja wa Vodacom nchini Tanzania

Dar es Salaam, Tanzania, Tarehe 25 Mei 2021: Mondia Pay na M-Pesa zimeshirikiana ili kuwawezesha Watanzania kufikia kwa rahisi zana maarufu za maudhui ya mtandaoni za Mondia kwenye mtandao wa huduma za dijitali wa Vodacom Tanzania PLC.

Bara la Afrika linashuhudia mfumuko wa teknolojia ya fintech. Kadri huduma za dijitali zinakita mizizi katika nchi nyingi, ndivyo muunganisho na ufikiaji wa vifaa unapongezeka na madhara ya janga la COVID-19 kusababisha wateja wengi kuingia mtandaoni. Kulingana na GSMA, thuluthi mbili ya shughuli za kimataifa za kutuma na kupokea pesa kupitia simu za mkononi zinaoongozwa na nchi za kusini mwa jangwa la sahara.

Mondia Pay imeunganisha huduma maarufu zaidi ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu ya mkononi ya Afrika na mfumo mkubwa zaidi wa fintech wa eneo, M-Pesa, na mtoa huduma maarufu zaidi wa Afrika wa burudani dijitali, Mondia.

Kwa sasa, zaidi ya wateja Milioni 7 wa Vodacom Tanzania wanaotumia Huduma za Bei Nafuu (VAS) na huduma za dijitali wanaweza kutumia masalio yao ya mjazo wa simu kupitia SMS na USSD ili kujisajili kwa huduma za dijitali za Mondia ikiwa ni pamoja na PlayInc., MyMuze, Ligi Kuu ya Vodacom, pamoja na huduma zingine nyingi za habari na burudani.

Mbali na chaguo la kufanya malipo la Mondia Pay na M-Pesa, sasa watumiaji wana njia salama na rahisi ya kulipa inayowaunganisha na maudhui bora zaidi ulimwenguni, kuanzia kwa spoti na filamu hadi kwa muziki na michezo. Ushirikiano huu unaonyesha uwezo wa ukuaji wa ubunifu wa teknolojia ya fintech na ushirikiano katika udhibiti wa maudhui na fursa kwa wauzaji na washirika wa kibiashara wa Mondia wa kufikia masoko mapya na fursa za kuchuma mapato.

“Mstakabali wa fintech unaenda kuongozwa na ushirikiano bunifu ambao unatoa huduma rahisi na zinazovutia kwa wateja. Tunajivunia zaidi juhudi zetu za kuwawezesha wateja kote nchini Tanzania kunufaika kutokana na ujumuishaji wa M-Pesa kwenye Mondia Pay kama njia ya ziada ya kulipa. Tunaunga pia mkono juhudi endelevu zinazochukuliwa ili kuleta mabadiliko katika jumuiya za huduma za kutuma na kupokea pesa kupitia simu za mkononi, ambazo zimezidi kuwa maarufu katika miezi 12 iliyopita,” alisema Simon Rahmann, Afisa Mkuu Mtendaji (CEO) wa Mondia Pay.



mondia.

Mkurugenzi wa Huduma za Dijitali wa Vodacom Tanzania Nguvu Kamando alisema, “Chaguo hili jipya la kulipa la M-Pesa, linalowezesha na Mondia ni kipengele muhimu zaidi cha ajenda yetu ya kufanikisha huduma za dijitali na linaongeza uwezo wa wateja wetu kufikia huduma za dijitali za Mondia. Matumizi ya M-Pesa, ambayo ni teknolojia maarufu zaidi ya huduma za kutuma na kupokea pesa kupitia simu za mkononi inayotumiwa na zaidi ya wateja milioni 13 nchini Tanzania yenye mtandao mkubwa zaidi wa majenti kote nchini, itaongeza na kurahisisha huduma za malipo kwa wateja wetu.”

Mwisho